

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
SHULE YA SEKONDARI MUBABA
S. L. P 185 BIHARAMULO – KAGERA**

FOMU A.

JINA LA MWANAFUNZI
ANWANI

**MAAGIZO RASMI YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2025 KATIKA SHULE
YA SEKONDARI MUBABA.**

1. Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kuijunga na kidato cha kwanza mwaka 2025 katika shule ya sekondari Mubaba. Nakupongeza na kukukaribisha.
2. Unatakiwa kuripoti shule kuanzia tarehe **13/01/2025** mpaka tarehe **31/01/2025** saa mbili asubuhi (02:00 asubuhi)
3. Shule ya sekondari Mubaba ni shule ya KUTWA (wanafunzi watakuwa wanakuja shulenii na kurudi kwao jioni)
4. Shule ya sekondari Mubaba ipo katika wilaya ya Biharamulo mkoani Kagera umbali wa kilometra 83 kutoka makao makuu ya wilaya. Shule hii iko kilometra 26 mashariki mwa mji mdogo wa Nyakanazi na kilometra 10 magharibi mwa mji mdogo wa Runzewe.

MAHITAJI YA LAZIMA KWA WANAFUNZI WOTE. A.

VIFAA VYA TAALUMA

- (i) Mwanafunzi aje na daftari (counter book Quire 3) zisizopungua kumi na tatu (13)
- (ii) Kalamu za wino na penseli za kutosha
- (iii) Mkebe wa hesabu (mathematical set)
- (iv) Mathematical table (four figure) (v) Aje na file aina ya Folder file

B. SARE ZA SHULE.

- i. Shati mbili nyeupe za mikono mifupi zisizo na urembo wa aina yoyote ile. Kwa Waislamu Hijabu ya rangi nyeupe.
- ii. Sketi mbili za rangi nyeusi zenye marinda makubwa manane, ndefu hadi kwenye kifundo cha mguu.(kwa wasichana)
- iii. Suruali mbili nyeusi zenye mfuko mmoja nyuma na marinda mawili mbele wala zisiwe modal au pisto.(kwa wavulana)
- iv. Soksi nyeupe ndefu jozi mbili
- v. Viatu vya Ngozi vya rangi nyeusi vya kufunga na Kamba
- vi. Begi dogo la kubebea daftari
- vii. T-shirt ya shule ya blue
- viii. Sweta la shule rangi ya maroon (damu ya mzee)
- ix. Track ya blue ya michezo
- x. Mkanda wa suruali rangi nyeusi usio kuwa na mitindo (kwa wavulana)
- xi. Tai moja ya rangi nyeusi

- C. Nimeambatanisha fomu mbili A na B fomu hizo zisomwe na zijazwe na kuletwa kwa mkuu wa shule, shule ya sekondari Mubaba. Siku atakapokuja kuripoti ni vyema aje na mzazi au mlezi wake.

Karibu sana

.....
Mkuu wa shule.

FOMU B.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

SHULE YA SEKONDARI MUBABA

S.L.P 185 BIHARAMULO

TAREHE.....

MGANGA MKUU WA WILAYA /ZAHANATI YA KATA.

Jina amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii ili kuendelea na masomo ni lazima apimwe kwanza.

Nitafurahi iwapo mbali na kupimwa kijana huyu ataangaliwa uwezo wa kuona wa macho yake. Kama ameshauriwa avae miwani hana budi kuinunua yeye mwenyewe kwa fedha zake. Tafadhari nijazie sehemu inayohusika chini baada ya kupima.

Asante kwa ushirikiano

.....

Mkuu wa shule

MKUU WA SHULE,

SHULE YA SEKONDARI MUBABA, S.L.P 185 BIHARAMULO.

Nimempima mwanafunzi aliye tajwa hapo juu na kuona kwamba ana matatizo /ugonjwa wa

A. Kifuakikuu.....

B. Macho.....

C. Masikio.....

D. Akili.....

E. Kilema.....

F. Choo(stool).....

G. Kwa wasichana tu ana / hana mimba.....

H. Mengineyo.....

Saini na muhuri wa ofisi.....

Mganga mkuu wa wilaya /zahanati ya kati